
Form C1

WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA JUNI HADI AGOSTI, 2026







Imeandaliwa na;


**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania
Phone: 0800114031 / 0800114032
E-mail: barua@wrbwb.go.tz
Website: www.wrbwb.go.tz

Mei, 2026

## 1. UTANGULIZI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha Mwezi Juni hadi Agosti,2026 ili wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kipindi cha Mwezi Juni hadi Agosti, 2026[1].




Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

### 1.1 ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA

Uwezekano wa kiasi cha maji kuwa juu ya wastani wa muda mrefu (2009-2024), hali inaweza kusababisha yafuatayo; -


- i. Kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, Barabara, miradi ya maji katika Mikoa ya Morogoro na Pwani
- ii. Uharibifu wa miundombinu na mali katika Mikoa ya Morogoro na Pwani


[1] Taarifa ya Mwelekeo wa Mvua zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa miezi mitatu ijayo kuanzia Juni -Agosti,2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.**

| Jina la Mto | Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji | Kielelezo |
|---|---|---|
| Ruvu | Utabiri unaonyesha mwelekeo wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kipindi cha Mwezi Juni – Agosti, 2026 utakuwa Juu ya Wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009 – 2024) pamoja na utabiri wa Mwaka 2025 kama inavyoonekana katika **Kielelezo,** hii ni kutokana na utabiri wa hali ya mvua kutoka TMA ambao unaonyesha kutakuwa na mvua zitakazo endelea kunyesha hadi Mwezi Agosti,2026 katika maeneo ya *Catchment*. Aidha, Utabiri unaoyesha kiasi cha maji kilichopo kwa sasa na baada ya miezi mitatu (Juni - Agosti 2026) kitatosheleza mahitaji ya sekta tajwa hapo juu ambayo ni mita za ujazo sita (6) kwa sekunde. |  |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | Utabiri unaonyesha kwa Kipindi cha Mwezi Juni -Agosti, 2026 wastani wa ujazo wa maji utafikia mita za ujazo milioni 468.3. Ujazo huu ungeweza kujaza Bwawa la Kidunda yenye uwezo wa mita za ujazo Milioni 190 kwa asilimia 100 kama Ujenzi wa Bwawa ungekuwa umekamilika. |  |

## 3. USHAURI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu inazishauri sekta za Kilimo, Madini, Ujenzi, Utalii, Ufugaji na Uvuvi, Viwanda na usambazaji maji majumbani kuzingatia mambo yafuatayo; -

### a) Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini (UWSSA) na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA)

Bodi inazishauri Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuchukua tahadhari dhidi ya uharibifu wa miundombinu unaoweza kujitokeza na kupelekea uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo yao.

### b) Makazi

Bodi inashauri wananchi kuendelea kuchukua hatua za ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba zao ili waweze kuyatumia kwa shughuli mbalimbali ikiwemo garden.

### c) Kilimo

Bodi inashauri sekta kufanya mambo yafuatayo; -

i. Kuvuna maji ya mvua kwa kutumia mabwawa yaliyojengwa/yanayojengwa ili kuyahifadhi maji mengi kipindi hiki na kuyatumia kipindi cha kiangazi kwa ajili ya umwagiliaji
ii. Wakulima wanashauriwa kuzingatia ushauri wa Maafisa Kilimo juu ya umwagiliaji wa mazao katika maeneo yao kwa kuzingatia kalenda ya umwagiliaji.
iii. Vilevile, Sekta iharakishe ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu zinazoendelea kujengwa.

### d) Ufugaji na Uvuvi

Bodi inashauri sekta kuchimba malambo ili kuhifadhi maji katika kipindi hiki cha maji mengi ili yatumike kipindi cha kiangazi kunyweshea mifugo. Pia, wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa mifugo katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo katika mpango wa matumizi bora ya ardhi zilizopo katika Halmashauri za Wilaya. Uvuvi wa kutumia sumu katika vyanzo vya maji hauruhusiwi.

**e) Madini**

Bodi inashauri Sekta ya Madini na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha uchimbaji na uchenjuaji wa Madini unafanyika nje ya vyanzo vya maji ili kulinda ubora wa maji kwa watumiaji mbalimbali.

**f) Ujenzi**

Bodi inasisitiza sekta kuchukua tahadhari dhidi ya kiwango cha maji kilichopo kwa miradi inayoendelea kutekelezwa ikiwemo Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili kutokuathiri utekelezaji wa mradi pamoja na usalama wa mradi kwa ujumla.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kufuatilia kwa ukaribu zaidi hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kufanya utabiri wa vipindi vifupi vya kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha wadau wake ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kuongezeka/kupungua wingi wa maji utakaoweza kujitokeza.